# JARIDA LA MWEZI


TOLEO NA. 057 JULAI 2025

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



1 BODI YA TMA YAFANYA ZIARA YA KIKAZI RADA YA HALI YA HEWA BANGULO, PUGU NA KITUO CHA HALI YA HEWA JNIA

2 DKT CHANG'A AFANYA MAZUNGUMZO YA KITAALAMU NA KATIBU MKUU WA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO)



3 FAHAMU ZAIDI:
HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI, 2025



KITAIFA

# BODI YA TMA YAFANYA ZIARA YA KIKAZI RADA YA HALI YA HEWA BANGULO, PUGU NA KITUO CHA HALI YA HEWA JNIA

**Dar es Salaam**



Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilifanya ziara ya kikazi ya kukagua utendaji kazi wa Mamlaka katika kituo cha Rada ya Hali ya Hewa, Bangulo, Pugu na Ofisi za TMA zilizopo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam, tarehe 23 Julai 2025. Ziara hiyo iliongozwa na Mwenyekiti wa Bodi Mhe. Jaji Mshibe Ali Bakari na Makamu Mwenyekiti, Dkt. Emmanuel Mpeta.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Jaji Mshibe alisema lengo la ziara ni kukagua na kutathmini usimamizi na utendaji kazi wa miundombinu ya TMA na kutathmini utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya Bodi katika kuboresha huduma na pia kutambua changamoto zilizopo, na kuona taasisi ilipo na inapoelekea. "Bodi imekuwa ikitoa maelekezo hivyo leo ilikuwa ni siku maalum kuangalia utekelezaji wake". Alisema Jaji Mshibe.

Alisisitiza kuwa TMA ya sasa imepiga hatua kubwa katika uboreshaji wa miundombinu ya utoaji huduma. Aidha, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuiwezesha Mamlaka kwa miundombinu ya kisasa.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC) Dkt, Ladislaus Chang'a aliishukuru Bodi kwa kutembelea na kujionea



utendaji kazi wa Mamlaka katika uangazi, uchakataji wa data na utoaji wa utabiri na kujionea miundombinu ya kisasa ambayo Serikali imeiwezesha TMA kuipata. Pia aliishukuru Bodi kwa maelekezo ambayo wamekuwa wakiyatoa kupitia vikao mbalimbali vya bodi, na kuiwezesha TMA kuendelea kuwa bora.

Akitoa ufafanuzi wa faida za uwekezaji wa miundombinu ya kisasa katika sekta ya hali ya hewa nchini alisema " Kupitia rada za hali ya hewa, Mamlaka imefanikiwa kuboresha utabiri wa hali ya hewa pamoja na kuendesha mafunzo ya rada kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati, wataalamu wa hali ya hewa kutoka nchi 10 za Afrika Mashariki na Kati walipata mafunzo mjini Mwanza , Tanzania na kuendelea kuipa heshima kubwa nchi yetu".

Aliongeza kwa kufafanua kuwa, Serikali imeendelea kuhakikisha usimamizi wa mitambo hii ya kisasa inakuwa endelevu kwa kuajiri na kuwezesha wataalamu kupata mafuzo husika, ambapo mpaka sasa TMA ina wahandisi 30.


Katika hatua nyingine wajumbe wa Bodi walipata fursa ya kutembelea Kompyuta Kubwa ya Kisasa (Computer Cluster) yenye uwezo mkubwa wa kuchambua na kuchakata taarifa za hali ya hewa na kuimarisha utoaji utabiri katika maeneo madogomadogo na mahsusi kwa haraka na usahihi zaidi.



KIMATAIFA

# DKT CHANG'A AFANYA MAZUNGUMZO YA KITAALAMU NA KATIBU MKUU WA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO)

**Geneva, Uswisi**



Katibu Mkuu wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (World Meteorological Organization - WMO) Prof. Celeste Saulo aliahidi kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) katika kuboresha huduma za hali ya hewa kwa matumizi katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Aliyasema hayo wakati wa kikao baina yake na Dkt. Ladislaus Chang'a, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika WMO na Makamu wa Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC) wakati wa kikao cha 69 cha Kamati Kuu Tendaji ya IPCC (Intergovernmental Panel on Climate Change-IPCC (69th IPCC Bureau), tarehe 02 Julai 2025 Jijini Geneva, Uswisi. Kikao hicho kilikuwa na lengo la kujadiliana kuhusu maendeleo ya utoaji wa huduma za hali ya hewa na mipango ya kuendeleza ushirikiano.

Prof. Celeste Saulo aliipongeza TMA kwa uwekezaji mkubwa katika sekta ya hali ya hewa kupitia Serikali hususan katika miundombinu ya kisasa ya hali ya hewa na kwa kuendelea kufanya vizuri katika utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini pamoja na kusaidia nchi nyingine katika sekta ya hali ya hewa. Prof. Celeste Saulo ameahidi kuendelea kusaidia katika kuboresha huduma za hali ya hewa na mafunzo kwa wataalamu wa hali ya hewa kupitia programu mbalimbali za WMO ikiwa ni pamoja na eneo la mafunzo ya akili mnemba (Artificial Inteligence-AI). Aidha, Prof. Saulo alisisitiza kuwa, Taasisi za hali ya hewa za nchi wanachama ndizo zenye jukumu mahsusi la kutoa huduma za hali ya hewa katika nchi wanachama wa WMO hivyo uwekezaji katika sekta hii utaboresha zaidi huduma hizi kwa jamii.

“ Taasisi za hali ya hewa kama TMA ndizo zenye jukumu mahsusi na chanzo cha kuaminika cha huduma za hali ya hewa kwa mujibu wa miongozo ya WMO na napongeza TMA kwa kuendelea kutumia vyema uwekezaji wa Serikali ya Tanzania kutoa huduma bora za hali ya hewa. Pia napongeza TMA kwa kuwa mstari wa mbele kusimamia vyema programu za WMO na kusaidia nchi nyingine kikanda ili kuboresha zaidi huduma za hali ya hewa katika nchi zao na kikanda” Alisema Prof. Celeste Saulo.

Katika Kikao hicho, Dkt. Ladislaus Chang’a alieleza dhamira ya TMA ya kuboresha huduma za hali ya hewa na kusimamia vyema programu za WMO zinazotekelezwa nchini na kikanda.

“TMA itaendelea kutoa wataalamu wake mahiri katika kuchangia utekelezaji wa programu mbalimbali za WMO kwa manufaa ya Dunia nzima na tutaendelea kusaidia wenzetu hasa katika kanda ya Afrika kwa uzoefu wa utaalamu tulio nao, kwa msaada wa WMO na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika sekta ya hali ya hewa nchini” Alisema Dkt. Chang’a.

Aidha, Dkt. Chang’a alimjulisha Katibu Mkuu wa WMO kuwa, Taasisi za Hali ya Hewa za Nchi wanachama wa WMO ambazo wataalamu wa TMA walitoa msaada wa kiufundi Barani Afrika hivi karibuni ni pamoja na Lesotho, Namibia, Burundi, Zimbabwe na Sudan Kusini, ambapo nchi hizo waliwezeshwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya uboreshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Ubora wa Huduma (Quality Management System-QMS and Competency Assessment), utabiri wa hali mbaya ya hewa, utabiri wa hali ya hewa kwa kutumia modeli za kihesabu/kompyuta (Numerical Weather Prediction-NWP), mchakato wa kisheria katika sekta ya hali ya hewa na usambazaji wa huduma za hali ya hewa kwa umma.

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY


## FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI, 2025

Kipindi cha mwezi Agosti 2025, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi, na viwango vya chini zaidi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Aidha, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu. Kwa upande wa mvua, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache, hususan yale yalioko ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 25 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Kwa maeneo ya nchi kavu kati ya nyuzi joto 14 °C na 22 °C. Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. **Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, huku vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 15 °C. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. **Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya baridi zaidi ya kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 °C inatarajiwa katika maeneo ya miinuko, ikijumuisha mkoa wa Njombe. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. **Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi pamoja na vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 °C . **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Katibu Mkuu wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Prof. Celeste Saulo (kushoto) katika picha ya pamoja na Dkt. Ladislaus Chang'a, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika WMO na Makamu wa Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC) wakati wa kikao cha 69 cha Kamati Kuu Tendaji ya IPCC (Intergovernmental Panel on Climate Change-IPCC (69th IPCC Bureau), tarehe 02 Julai 2025 Jijini Geneva, Uswisi.*



*Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Mhe. Jaji Mshibe Ali Bakari (kushoto) pamoja na wajumbe wa bodi na menejimenti ya TMA, wakipata maelezo ya utendaji kazi wa Mamlaka katika kituo cha Rada ya Hali ya Hewa, Bangulo, Pugu wakati wa ziara ya Bodi iliyofanyika tarehe 23 Julai, 2025.*





*Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), pamoja na Menejimenti ya TMA, wakipata maelezo kuhusu ufanisi wa kompyuta ya kisasa (Computer Cluster (kushoto)) na utendaji kazi wa kituo cha uangazi cha hali ya hewa (kulia) kilichopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, wakati wa ziara ya Bodi iliyofanyika tarehe 23 Julai, 2025.*


JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 056
JUNI 2025
TMA
1 MKUU WA MAKAPTENI ZANZIBAR AELEZEA MIPANGO YA SAFARI INAVYOTEGEMEA TAARIFA ZA HALI YA HEWA
2 DKT. CHANG'A ASHIRIKI MKUTANO WA 62 WA KAMATI YA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI
3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2025
ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga


**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa



www.meteo.go.tz

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline_TV

WhatsApp channel
**Tanzania Met Authority**

Scan hapa kujiunga

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.